**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHISENGA

**Julai, 2024**

**KALAMBO - RUKWA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Email: chisenga.kalambo@gmail.com**

**Namba za Simu: 0746 631 934**

**Mkuu wa Shule: 0754 418 957**

**Makamu Mkuu wa Shule:0625 522 286**

**Matron: 0764 879 227**

**Shule ya Sekondari CHISENGA**

**S.L.P. 752**

**Tarehe ....................……………**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi …………..………………………………**
**S.L.P ……………………………………..**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI CHISENGA HALMASHAURI YA KALAMBO MKOA WA RUKWA MWAKA 2024**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024 na atasoma tahasusi ya............(**HGL, HKL, HGLi, HGFa**)
Shule ya Sekondari CHISENGA ipo umbali wa Kilometa 103 kusini magharibi ya mji wa Sumbawanga. Usafiri wa basi kutoka mjini SUMBAWANGA unapatikana katika kituo kikuu cha mabasi mkoani (KATUMBA) Na kituo kidogo cha mabasi cha (SOKO MATOLA) Nauli ni Shilingi 5000/= kutoka Sumbawanga mjini mpaka shuleni. Magari ya moja kwa moja hadi shuleni ni pamoja na ya kampuni za AZUNA, MAMBWE EXPRESS, B.S na IPAD yanayoelekea mji maarufu wa Kasanga kati ya saa 4 hadi saa 7 mchana kila siku na kumufikisha mwanafunzi hadi shuleni CHISENGA (KISUMBA).

Muhula wa Masomo unaanza mwezi JULY, hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 1/07/2024 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 15/07/2024

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

**(a) Wavulana**

i. Suruali mbili (moja ya rangi ya **KIJANI ILIYOIVA** na nyingine rangi ya **KAKI)**.
ii. **Mshono wa suruali:** iwe na mifuko mitatu mmoja nyuma upande wa kulia na miwili pande zote kulia na kushoto pembeni **na siyo yakubandika**,iwe na rinda mbili kila upande na upindo wa chini (miguuni) ugeuzwe juu (turn up), upana miguu ni uwe wa kutosha isiwe ya kubana.
iii. Mashati mawili meupe mikono mirefu
iv. Viatu vya ngozi vyeusi vya kufunga kamba
v. Sweta la rangi ya **KIJANI JESHI**. lenye ukosi wa V.
vi. Soksi nyeusi jozi mbili
vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali.
viii. Tai mbili. (Moja Rangi ya **KIJANI ILIYOIVA** na nyingine **KAKI**)
ix. T- shirt ya shule moja yenye nembo ya shule inayouzwa huku.
x. Suruali nyeusi mbili za vitambaa za kushindia. (shamba dress)





**(b) Wasichana**

i. Sketi mbili zenye marinda kumi na mbili (moja Rangi ya **KIJANI ILIYOIVA** na nyingine **KAKI**).
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu
iii. Viatu vyeusi vya ngozi vya kufunga kwa kamba vyenye kisigino kifupi
iv. Soksi nyeupe jozi mbili
v. Sweta la Rangi ya **KIJANI JESHI** lenye ukosi wa V.
vi. Tai mbili (Moja ya rangi ya **KIJANI ILIYOIVA** na nyingine Rangi **KAKI**)
vii. Rangi ya Hijab ni nyeupe ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifungo cha mkono akisimama.

viii. Gauni mbili za kushindia (shamba dress) kitambaa cha draft ndogo rangi ya blue/nyeupe.



ix. T- shirt ya shule moja yenye nembo ya shule inayouzwa huku.





**(c) Kwa Waislam.**

Rangi ya hijabu ifanane na rangi ya sare ya shule.

**(d) Sare ya michezo kwa shule hii ni:-**

**Wavulana:**

i. Raba za michezo jozi moja.
ii. Bukta rangi ya blue au truck suit rangi ya blue

**Wasichana:**

i. Raba za michezo jozi moja.
ii. Awe na truck suit rangi ya blue.

## NB: Nguo zisizokuwa sare ya shule haziruhusiwi shuleni.

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari counter book quire 4 ziwe nane (8)
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Mwanafunzi aje na Vitabu vya masomo ya tahasusi husika na General studies.
iv. Scientific Calculator kwa wanaosoma somo la Geographia katika tahasusi zao.
v. Godoro upana futi mbili na nusu (***futi 2.5)***
vi. Mashuka(blue bahari) Jozi 2, blanket 1, foronya ya godoro 1, chandarua 1
vii. Nguo za ndani za kutosha;
viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
ix. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
x. (a) Jembe 1 na fagio chelewa 1 kwa **HGL**
(b) Soft bloom 1 na kwanja 1 kwa **HKL**
(c) Reki 1 na kwanja 1 kwa **HGLi**
(d) Jembe 1 na Hard bloom 1 kwa **HGFa**
xi. Sanduku la chuma moja lenye kufuri kwa ajili ya kutunzia vitu vyake(Trunker).
xii. Bima ya afya ya NHIF au CHF inayotolewa na wizara ya afya kwa gharama ya 5000/= (Jukumu la Bima ya NHIF mzazi awajibike mwenyewe, Bima ya CHF shule inaweza kushughulikia).
xiii. Aje na result slip ya matokeo ya kidato cha nne.
xiv. Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa.

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII**

THE HEADMASTER
CHISENGA S.S
KALAMBO

**JOSEPH R. MAGOGO**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule : JOSEPH R MAGOGO 0754 418 957**
- **Makamu Mkuu wa Shule: POLELA .M 0625 522 286**
- **Mwandamizi Taaluma : KITUHILE .J 0764 879 227**
- **Mwandamizi Malezi : MBASELA .J 0763 299 549**

## VITABU VYA KUJA NAVYO

Mwanafunzi anatakiwa kuja na vitabu kutegemeana na tahasusi alivyochaguliwa kusoma. Ifuatavyo ni orodha ya vitabu kutegemeana na tahasusi zilizopo hapa shuleni.

❖ **GENERAL STUDIES**

General studies for form five (v) & six (vi). By Richard R. F. Mbalase (2011) General studies for Advanced level certificate, Afroplus industries Ltd.

❖ **ENGLISH LANGUAGE A – LEVEL.**

- An enemy of the people: By Henrik Ibsen
- Advanced English Literature: By Nyambali Nyangwine (literature analysis)
- A man of the people: By Ngugi wa Thiong'o
- Oxford Advanced English (oxford 2015)
- Advanced English language: By kadeghe M (2015)
- Advanced English language New syllabus: By Nicolous Ashel (2016….)
- The Beautiful Ones Are Not Yet Born: By Ayi Kwei Armal.

❖ **GEOGRAPHY.**

- Practical geography for Africa; Longman Group: Hong Kong: By Pritchard S.M (1990).
- General geography in Diagram's: peason education south Asia ptc Ltd Singapore: By Bunnett R.B 2006).
- Geography an integrated Approach: Nelson Thornes Ltd; Delta place 27 Bath Road; united Kingdom: By Waugh D(2009).
- Physical geography: MC cram Hill-New york: By Carlson H.D. Mcheary D. and Plummer C. C (1997).
- Human and Economic geography: Oxford University press; united kingdom: By Leong C. G. Morgan C, G (2009).
- Principles of physical geography: by Monk House F. J (1975

❖ **HISTORY**

1. Modern word History by Ben Warsh
2. Africa in the world History by Nyirenda
3. The Russian Revolution and the Bolshevik
4. Major events in the Africa History by Fr. Kamara
5. Zamani East Africa History by Ogot and J.A Kieban

❖ **KISWAHILI.**

1. Kunga za fasihi na lugha (Msokile m. 1992) EDP
2. Historia ya Kiswahili Africa Mashariki (Shiragdin na Mnyapala)
3. Kunga za ushairi na Diwani yetu (Mlokozi M. na Mnyapala)
4. Sarufi ya Kiswahili sekondari na vyuo (Mdee) DUP – DSM
5. Ndimi na Hisia za wabakiki katika kioo cha lugha - DSM (Senkoro 1973)
6. Kamusi ya Kiswahili Sanifu – TUKI

- **GENERAL STUDIES MODULE – Bulyaga stationary Sumbawanga@ 5000/=**
- **GEOGRAPHY MODULE 1 - Bulyaga stationary Sumbawanga@ 5000/=**
- **GEOGRAPHY MODULE 2 - Bulyaga stationary Sumbawanga@ 5000/=**
- **HISTORY MODULE 1 - Bulyaga stationary Sumbawanga@ 5000/=**
- **HISTORY MODULE 2 - Bulyaga stationary Sumbawanga@ 5000/=**

**HISTORIA YA MWANAFUNZI:**

Jina la mwanafunzi……………………………………………
Jina la baba …………………………………………..
Jina la mama ……………………………………………
Shule aliyohitimu kidato cha nne………………………………………………………..
Mtaa/Kijiji atokacho ……………………………………………
Tarehe ya kuzaliwa …….................. Dini …………………Dhehebu …………………..
Kabila …………………………….

**UTHIBITISHO:**

**5.1 Ahadi ya Mwanafunzi**

Mimi …………………………………………………………… nakubali nafasi niliyopewa ya kujiunga na kidato cha …………… mwaka …………. Katika shule ya Sekondari Chisenga na ninaahidi:-

i. Kuzingatia taratibu na kanuni zote za shule
ii. Kuweka bidii katika masomo yote
iii. Kushiriki katika shughuli za elimu ya kujitegemea
iv. Kuwa na nidhamu ya juu ndani na nje ya shule

**Jina ……………………………………………………………….**
**Sahihi …………………………………**
**Tarehe ………………………………...**

**5.2 Ahadi ya Mzazi / Mlezi**

Mimi ……………………………………… mzazi / mlezi wa …………………………..
Naahidi kwamba:

i. Nitatimiza gharama za mwanangu kama nilivyoelekezwa
ii. Nitamhimiza mwanangu kuzingatia taratibu za shule pamoja na masomo
iii. Nakubaliana na kanuni na sheria zilizotolewa na serikali juu ya mwanafunzi (mwanangu)

**Jina …………………………………………………………………**
**Sahihi ………………………………**
**Tarehe ……………………………...**

**PRESIDENT’S OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

CHISENGA SECONDARY SCHOOL,

P.O.BOX 752,

**KALAMBO – RUKWA.**

DATE …………………..

MEDICAL OFFICER:

………………………………………………………………

……………………………………………………………….

………………………………………………………………

## REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Please examine……………………………………………………….as to his/her fitness.

1. Hemoglobin……………………………………………………………………………..
2. P.V Bleeding……………………………………………………………………………
3. Blood Pressure………………………………………………………………………….
4. Blood Group…………………………………………………………………………….
5. (a) Sight…………………………………………………………………………………
   (b) Hearing……………………………………………………………………………
6. Urine for pregnancy…………………………………………………………………….
7. Stool for routine examination…………………………………………………………
8. Asthma……………………………………………………………………………………….
9. Skin disease………………………………………………………………………………….
10. Leprosy……………………………………………………………………………………….
11. Epilepsy………………………………………………………………………………………
12. Pulmonary Tuberculosis……………………………………………………………..
13. Deformity…………………………………………………………………………………
14. Mental problem…………………………………………………………………………..
15. V.D (GVE TYPE)……………………………………………………………………
16. Any other serious disease (not mentioned above)
…………………………………………………………………………………......................
…………………………………………………………………………………………………….
17. Check pregnancy………………………………………………………………………...
18. MRDT…………………………………………………………………………………..

COMMENTS
………………………………………………………………
……………………………………………………………..
………………………………………………………………

NAME/SIGNATURE
……………………………
…………………………….
…………………………….

**STAMP**